



BUSINESS PLAN

SIMPLIFIED SWAHILI TEMPLATE

Haya ni maelezo mafupi ya jinsi ya kuandaa mpango wa biashara (business plan) kwa Kiswahili. Lugha rahisi imetumika kuandaa nyaraka hii. Usomo wa dakika 5.

Abdurahman Suddy

suddycontact@gmail.com

+255 656 312 675

Twitter @AbdulSudi

❖ Executive Summary

Hichi ni kipande kidogo kinacho fupisha mpango wa biashara yako nzima, vile vitu muhimu ambavyo vitaonekana kwenye mkakati wako (business plan) utaviandika hapa. Hichi ni kipande cha mwisho kuandikwa lakini kinawekwa cha kwanza. Kinamrahishia mtu anaetaka kupata picha ya mkakati wako kwa haraka haraka bila kusoma nyaraka nzima.

❖ Company/ Business Description

Hapa unaieleza kampuni yako, kampuni imeanzishwa lini, inafanya biashara gani, kina nani wanaimiliki hiyo kampuni, nk.

❖ Product/Service

Hapa utaeleza bidhaa yako kwa kina, utaelezeza ikoje, ina vitu gani, in uwezo gani, kwanini wateja wanunue ya kwako. Jina la bidhaa yako, itaonekanaje na picha yake ikiwezekana.

❖ Marketing Plan

Hapa utaeleza wateja wako kinani yaani unawalenga watu gani. Halafu utaeleze utawapata wapi na bei zao. Jinsi gani utaitangaza biashara yako. Vile vile utaeleza uwezo wa kampuni yako au mwenyewe kuweza kuifanya hiyo biashara, madhaifu yako, tahadhari zake, na fursa ulizonazo (S.W.O.T analysis).

Utaeleza pia jinsi gani utapanga bei za bidhaa yako, vile vile jinsi gani utasambaza bidhaa zako.

Hapa tena utaeleza washindani wako kina nani, wana uwezo gani, na wana madhaifu gani na jinsi gani unapanga kuwashinda wapinzani wako kwenye soko la hiyo biashara.

❖ Management of the Business/ Company

Hapa utaeleza jinsi gani utaisimamia biashara yako, utakuwa na wafanya kazi wangapi, hao wafanyakazi wanafanya shughuli gani kuweza kusaidia bidhaa iendee sokoni, na mfumo mzima wa utawala.

Pia utaangalia unawalipa shilingi ngapi biashara yako endelee mbele bila hasara.

❖ Operation Plan

Hapa utaonesha jinsi gani utaitengeneza hiyo bidhaa au hiyo huduma unaitoaje, kila kitu ambacho kinatakiwa kifanyike kinatakiwe kioneshwe hapa. Kuanzia unapopata malighafi mpaka bidhaa inakamilika.

❖ Start-Up Capital

Hapa utaonesha unahitaji shilingi ngapi ili biashara ianze, vili vile utapata wapi hiyo pesa. Kama ya mkopo inabidi ioneshwe inatoka wapi, inarudishwa lini na riba yake na kila kitu. Kama ya wawekezaji inabidi uioneshwe hao wawekezaji wana pata hisa ngapi kwenye hiyo biashara (equity au share).

❖ Financial Plan

Hapa utaonesha jinsi gani utaitumia hiyo pesa, kila tumizi utalionesha, fedha zinazotoka na kuingia zote utazianzisha (Inflow & outflow). Maanisho ya matumiza ya mwanzo mpaka ya mwisho wa mwaka yataelezwa hapa. Haya ni makadirio tu.

❖ Financial Projection

Hapa unakadiria mapato na matumizi ya mbeleni kama ni baada ya mwezi, mwaka au miaka 3 na kuaendelea. Hii ni muhimu ili kujua biashara yako ina faida mbeleni au hapana. Hapa utaonesha kama biashara inakuwa au la.

❖ Way Forward/ Immediate action

Hapa utamalizia kwa kuonesha unaanza na kitu gani kukifanya ili bishara yako ianze kwa muda huo unapoamua kuanza.

~BIASHARA NJEMA~